



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu. 03-3425-4531 FAX. 03-3425-7844
TELEGRAPHIC ADDRESS TANZANREP-TOKYO
Barua pepe: tzrepjp@tanzaniaembassy.or.jp
tokyo@nje.go.tz

UBALOZI WA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA
21-9, KAMIYOGA 4-CHOME
SETAGAYA-KU, TOKYO 158-0098

TAARIFA YA FURSA YA MASOMO NGAZI YA UMAHIRI, PROGRAM YA UCHUMI NA SERA YA UMMA KATIKA CHUO KIKUU TSUKUBA NCHINI JAPAN KWA MWAKA 2025 - 2027

Ubalozi umepokea taarifa kutoka Chuo Kikuu Tsukuba kilichopo nchini Japan kuhusu fursa za masomo ngazi ya Umahiri, Program ya Uchumi na Sera ya Umma kwa Mwaka wa Masomo 2025 – 2027 (Master's Program in Economic and Public Policy 2025 – 2027), inayotolewa chuoni hapo.

Dirisha la maombi ya kujiunga na masomo (Program Admission) litafunguliwa kwa utaratibu ufuatao:

- i) **1 Oktoba – 15 Novemba 2024:** Kwa ufadhili wa Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Asia (World Bank/ Asia Development Bank Scholarships): na
- ii) **2 Desemba 2024 – 17 Januari 2025:** Kwa ufadhili unaotolewa na Serikali ya Japan kupitia JICA / MEXT; au kwa ufadhili binafsi (self-funded).

Ubalozi unawasilisha taarifa hii ya fursa ya masomo inayotolewa na Chuo Kikuu Tsukuba, Japan ili kuwezesha watazania kuchangamkia fursa hiyo.

Watazania wenye nia, vigezo na sifa, wanashauriwa kujiandaa mapema na kujiweka tayari kwa maombi ya Program hiyo mara baada ya dirisha la maombi kufunguliwa. Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea:

Admission: <https://pepp.hass.tsukuba.ac.jp/admission/>

Tunashukuru kwa ushirikiano.

**UBALOZI WA TANZANIA
TOKYO
13 AGOSTI 2024**